**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

WIZARA YA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI

# MUHTASARI WA MAFUNZO YA UALIMU NGAZI YA CHETI ELIMU YA MSINGI

## SOMO LA UALIMU

**2009**

Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi, 2009

ISBN……………………………………………………….

Haki zote zimehifadhiwa. Hairuhusiwi kuiga, kunakili, kupiga chapa au kutoa kwa namna yoyote ile muhtasari huu bila idhini ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi.

Umebuniwa na kutayarishwa na:
Taasisi ya Elimu Tanzania
S.L.P. 35094
Dar es Salaam
TANZANIA

Tel. + 255 – 22 2773005,
Fax: + 255 22 2774420
E-mail: director.tie@tie.go.tz
Website: www.tie.go.tz

## IDHINI

Mafunzo ya Ualimu wa Elimu ya Msingi Ngazi ya Cheti ni ya miaka miwili na yamekusudiwa kuandaa walimu mahiri wenye uwezo wa kufanya kazi kwa dhati. Walimu hao watafundisha katika shule za msingi. Mwalimu mwanafunzi atatambuliwa kuwa ni mwalimu baada ya kuhudhuria na kufaulu mafunzo ya cheti ya miaka miwili ambamo pia atafanya na kufaulu mazoezi ya kufundisha.

Andiko hili linaidhinishwa kuwa ni **Muhtasari wa Somo la Ualimu wa Elimu ya Msingi Ngazi ya Cheti** wa mwaka 2009.

**Umeidhinishwa na ......................................................**

**Saini...................................................................**

**Tarehe...................................................................2009**

**Kamishna wa Elimu**
Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi
S.L.P 9121
**Dar- es-Salaam**

Simu: +255 222 110150, 110179, 11046
Nukushi: +255 222 113271
Wovuti: www.moe.go.tz

## YALIYOMO

**Ukurasa**

**UTANGULIZI**.......................................................................................... iv

Maelezo kuhusu Muhtasari iv

Madhumuni ya Mafunzo ya Ualimu Ngazi ya Cheti....................................... iv

Ujuzi wa Somo la Ualimu.............................................................................. v

Malengo ya Somo la Ualimu............................................................................. vi

Muundo wa Muhtasari........................................................................................ vi

Upimaji na Tathmini ya Maendeleo ya Mwanachuo ....................…………... vii

Muda wa Mafunzo……………………………………………………….. vii

**MADA**

Saikolojia........................................................................................................ 1

Makuzi na Ukuaji wa mtoto............................................................................ 2

Nadharia za Kujifunza..................................................................................... 5

Ushauri na Unasihi........................................................................................... 9

Mtaala............................................................................................................... 12

Matayarisho ya Ufundishaji............................................................................. 13

Ufundishaji........................................................................................................ 17

Upimaji Katika Elimu....................................................................................... 21

Tathmini katika Elimu...................................................................................... 25

Utafiti wa Kielimu............................................................................................ 26

Taaluma ya Ualimu.......................................................................................... 28

Maendeleo ya Elimu Tanzania......................................................................... 31

Uongozi wa Elimu Tanzania............................................................................ 33

Elimu Jumuishi................................................................................................ 34

Elimu ya Watu Wazima.................................................................................... 36

Rejea Zilizotumika........................................................................................... 38

## UTANGULIZI

### Maelezo kuhusu Muhtasari huu

Muhtasari huu ni kwa ajili ya somo la Ualimu ngazi ya Cheti. Umeandaliwa ili kumwezesha kila mkufunzi na mwanachuo wa Ualimu ngazi ya Cheti kuelewa mambo muhimu ya kufundisha na kujifunza.

Kuandaliwa kwa muhtasari huu kunatokana na uamuzi wa serikali wa mwaka 2008 wa kuimarisha mafunzo ya ualimu ili kuwajengea walimu na wanafunzi ujuzi na uelewa wa kutosha katika somo la Ualimu. Ili kutimiza azma hii, muhtasari huu umeundwa ili kumwezesha mwanachuo kupata fursa ya kuelewa mambo muhimu na ya msingi kuhusu elimu na kazi ya ualimu.

Muhtasari huu unachukua nafasi ya mihtasari ya masomo manne ya Ualimu ya mwaka 2003 ambayo ni Misingi ya Elimu, Mitaala na Ufundishaji, Upimaji, Tathmini na Utafiti na Saikolojia ya Elimu. Muunganisho huu unalenga kupunguza idadi ya masomo yanayofundishwa katika Kozi ya Ualimu ngazi ya Cheti.

Pamoja na masomo hayo manne yaliyounganishwa, muhtasari huu pia umezingatia:-

- Masuala mtambuko;
- Elimu ya Watu Wazima;
- Elimu maalum/Jumuishii;
- Uongozi wa Elimu;
- Wajibu na haki za Walimu.

### Sababu za kuwa na Muhtasari huu

Muhtasari huu umeandaliwa kumwezesha kila mwanachuo wa ualimu ngazi ya cheti kuielewa kazi yake kinadharia na kivitendo. Muda wa mafunzo ni miaka miwili chuoni. Muhtasari huu

umeandaliwa kutokana na uamuzi wa Serikali kupitia Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi 2008 wa kuimarisha mafunzo ya ualimu na kutatua tatizo la upungufu wa walimu ngazi ya cheti linalokabili nchi kwa ujumla. Hii ni pamoja na kukidhi mahitaji na idadi ya walimu kutokana na kupanuka kwa sekta ya elimu ya msingi kufuatia kutekelezwa kwa mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Msingi (MMEM), kuongezeka kwa mahitaji ya walimu wenye kiwango cha juu cha taaluma na utaalam na kushughulikia masuala mtambuko.

**Madhumuni ya Mafunzo ya Ualimu Ngazi ya Cheti**

Mafunzo ya ualimu hapa nchini yana madhumuni yafuatayo:

a) Kuwezesha wanachuo kupata nadharia ya saikolojia ya elimu na kunasihi.

b) Kuwawezesha wanachuo kupata stadi mbalimbali za kufundishia na kujifunzia.

c) Kukuza uelewa na uchambuzi wa mitaala itumikayo katika shule za msingi.

d) Kukuza na kuendeleza utaalam wa kufundisha masomo ambayo wanachuo watatakiwa kuyafundisha.

e) Kuwajengea wanachuo stadi na ujuzi wa kufanya utafiti wa kielimu, upimaji na tathmini.

f) Kukuza uwezo wa wanachuo katika uongozi na utawala wa kielimu.

g) Kukuza uwezo wa wanachuo juu ya kushughulikia masuala mtambuka.

h) Kuwajengea uwezo wanachuo wa kutumia TEHAMA katika mchakato wa kufundisha na kujifunza

i) Kubuni, Kutengeneza na kufaragua nyenzo za kufundishia na kujifunzia katika elimu ya Msingi.

j) Kujengea uwezo wanachuo wa kufanya utafiti kuhusu wanafunzi ili kuwabaini na kuwasaidia wale wenye mahitaji maalum katika shule za Msingi.

**Ujuzi wa somo la Ualimu**

Baada ya miaka miwili ya mafunzo ya ualimu ngazi ya cheti, mwanachuo aweze kuonesha kanuni za msingi, stadi na mwelekeo katika:

a) Kupanga na kuendesha mchakato wa ufundishaji.

b) Kupima na kutathmini maendeleo ya ufundishaji.

c) Kupanga na kusimamia darasa lake

d) Kufanya tafiti mbalimbali kwa lengo la kuboresha mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji

Kushauri na kunasihi wanafunzi wenye mahitaji maalumu katika ujifunzaji wao

**Malengo ya Somo la Ualimu**

Baada ya kumaliza mafunzo ya ualimu ngazi ya Cheti Mwanachuo aweze:

a) Kutumia mbinu za saikolojia katika kuchambua na kuelewa tabia za wanafunzi kieleimu na kimaisha.ili kuwawezesha kujifunza kwa ufanisi
b) Kutumia mbinu na stadi za kunasihi katika kurekebisha mienendo na tabia za wanafunzi ili waweze kujifunza kwa ufanisi.
c) Kutumia nadharia mbalimbali za kujifunza katika ufundishaji na ujifunzaji.
d) Kupata maarifa na stadi za utafiti katika kufanikisha ufundishaji na ujifunzaji.
e) Kutumia stadi za upimaji na tathmini ili kuboresha ufundishaji na ujifunzaji.
f) Kukuza uelewa na stadi zinazohusu saikolojia ya elimu jumuishi na ya elimu ya watu wazima.
g) Kuchambua mwelekeo wa falsafa na maendeleo ya elimu nchini Tanzania.
h) Kuelewa maarifa na stadi zinazohitajika katika uongozi wa elimu na uendeshaji wa shule
i) Kukuza uelewa na taaluma ya ualimu na vyombo vinavyomlinda mwalimu kazini.
j) Kutumia ujuzi wa mitaala katika kutayarisha masomo na kuyafundisha.
k) Kuwatambua watoto wenye mahitaji maalum na kubuni mbinu za kuwasaidia wajifunze vizuri.
l) Kupata maarifa na stadi ya uongozi na utawala wa Elimu

**Muundo wa Muhtasari**

Muhtasari huu una mada kuu 15 zilizochaguliwa kwa kuzingatia umuhimu na kiwango cha uelewa wa mwanachuo ngazi ya Cheti. Mada hizi zimepangwa katika mtiririko wenye mantiki na kila moja imegawanyika katika mada ndogo kurahisisha ujifunzaji na ufundishaji wa somo. Mada ndogo katika kila mada kuu imeambatanishwa na muda, malengo mahususi, mapendekezo ya mbinu za kujifunzia na kufundishia na upimaji katika mfululizo wa wima.

Mkufunzi wa somo hili anashauriwa kutumia mbinu zinazolenga kumshirikisha mwanachuo na kukuza uwezo wake wa kufikiri na kutumia maarifa anayojifunza katika mazingira tofauti. Mkufunzi anatakiwa kuwa mbunifu katika kutumia mbinu zilizopendekezwa na nyingine kulingana na hali halisi ya mazingira yake yaani somo lenyewe, uwezo wa wanachuo na muda.

Vile vile mkufunzi wa somo hili anashauriwa kutumia vifaa vitakavyomwezesha mwanachuo kushiriki kikamilifu katika tendo la kujifunza. Baadhi ya vifaa vimependekezwa katika kila mada ndogo na mkufunzi anatakiwa kuwa mbunifu kuwashirikisha wanachuo katika kutafuta vifaa vinavyofaa zaidi katika kuboresha ufundishaji na ujifunzaji.

**Upimaji na Tathmini ya Maendeleo ya Mwanachuo**

Wanachuo watapimwa mara kwa mara kwa kutumia mbinu anuwai za upimaji ili kufahamu maendeleo ya ujifunzaji wao. Upimaji huu utakuwa katika makundi makuu mawili. Upimaji Endelezi ambao utakuwa na jumla ya alama **50%** na Upimaji tamati utakaohusisha mitihani ya mwisho inayotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa (NECTA) nao utakuwa na jumla ya alama **50%.** Mazoezi ya kufundisha (BTP) yatapimwa kwa kuzingatia taratibu za Baraza la Mitihani la Taifa.

**Mchanganuo wa Vipengele vya Upimaji**

| **Na.** | **Mbinu za Upimaji** | **Mwaka wa Kwanza** | | **Mwaka wa Pili** | | **Idadi** | **Alama %** |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | **Muhula wa I** | **Muhula wa II** | **Muhula wa I** | **Muhula wa II** | | |
| 1 | Uwasilishaji darasani | 1 | 1 | 1 | 1 | 4 | 10 |
| 2 | Majaribio | 1 | 1 | 1 | 1 | 4 | 10 |
| 3 | Kazi za kila mwanachuo au Uandishi wa Insha | 1 | 1 | 1 | - | 3 | 05 |
| 4 | Kazi Mradi | | 1 | 1 | - | 2 | 05 |
| 5 | Mitihani ya mwisho wa mihula | 1 | 1 | 1 | | 3 | 20 |
| | Jumla ya Alama za Upimaji Endelezi | | | | | | 50 |
| 6. | Mtihani wa mwisho | - | - | - | 1 | | 50 |
| Jumla ya Alama za Upimaji Endelezi na Tamati | | | | | | | 100 |

**Muda wa Mafunzo**

Muda wa mafunzo ya Ualimu Ngazi ya Cheti ni miaka miwili (2) chuoni. Somo la Ualimu limepangiwa muda wa saa mbili tu kwa wiki. Mazoezi ya ufundishaji (BTP) yatafanyika katika muhula wa pili kwa mwaka wa kwanza na muhula wa kwanza kwa mwaka wa pili kwa muda

wa wiki nne nne. Katika kipindi chote cha mafunzo chuoni, mkufunzi anatakiwa azingatie umuhimu wa muda uliopangwa bila kuruhusu njia yoyote ya kupunguza muda huo. Iwapo muda utapungua mkufunzi atafute utaratibu wa kufidia. Mwaka wa pili utahitimishwa kwa mtihani wa taifa.

## 1. 0 SAIKOLOJIA

### 1.1 Dhana ya Saikolojia.

**Muda: Saa 2**

**Malengo Mahsusi**

Baada ya kukamilisha mada ndogo hii, mwanachuo aweze:-

Kueleza maana ya Saikolojia;

Kubainisha matawi ya Saikolojia

**Mbinu za Kufundishia na Kujifunzia**

Bungua bongo.

Majadiliano na mawasilisho kuhusu maana ya neno saikolojia na matawi yake.

**Vifaa vya Kufundishia na Kujifunzia**

a) Vitabu vya Saikolojia

b) Chati yenye kuonesha matawi ya saikolojia (Mti wa Saikolojia).

**Upimaji**

a) Maswali ya ana kwa ana kueleza maana ya neno saikolojia.

b) Kazi binafsi kubainisha matawi ya saikolojia.

### 1.2 Dhana ya Saikolojia ya Elimu.

**Muda: Saa 2**

**Malengo Mahsusi**

Baada ya kukamilisha mada ndogo hii mwanachuo aweze:

a) Kueleza maana ya Saikolojia ya Elimu;

b) Kutofautisha Saikolojia ya Elimu na matawi mengine ya Saikolojia;

c) Kueleza umuhimu wa Saikolojia ya Elimu kwa mwalimu na kwa mwanafunzi.

**Mbinu za Kufundishia na Kujifunzia**

a) Maswali na majibu.

b) Majadiliano katika vikundi.

c) Majadiliano katika jozi na mhadhara shirikishi.

**Vifaa vya Kufundishia na Kujifunzia**

a) Vitabu vya saikolojia

b) Majarida ya saikolojia

c) Makala mbalimbali za utafiti wa kielimu.

**Upimaji**

a) Zoezi kueleza umuhimu wa saikolojia ya elimu.

b) Kazi binafsi kutofautisha saikolojia ya elimu na matawi mengine ya saikolojia.

c) Mkoba wa kazi

## 2.0 MAKUZI NA UKUAJI WA MTOTO

### 2.1 Dhana ya Makuzi ya Mtoto.

**Muda: Saa 2**

**Malengo Mahsusi**

Baada ya kukamilisha mada ndogo hii, mwanachuo aweze:-

a) Kueleza maana ya makuzi ya mtoto;

b) Kuelezea umuhimu wa kujifunza makuzi ya mtoto;

c) Kufafanua wajibu wa familia na jamii nzima katika kuendeleza makuzi ya mtoto;

d) Kutofautisha ukuaji na makuzi ya mtoto.

**Mbinu za Kufundishia na Kujifunzia**

a) Bungua bongo.

b) Majadiliano kufafanua wajibu wa familia na jamii katika makuzi ya mtoto.

c) Maswali na majibu.

**Vifaa vya Kufundishia na Kujifunza**

a) Vitabu na majarida yanayohusu malezi ya mtoto na makuzi yake.

b) Kazi za maktaba/Mtandao

**Upimaji**

a) Jaribio.
b) Chemsha bongo.
c) Kazi mradi kufafanua wajibu wa familia na jamii katika makuzi ya mtoto.

## 2.2 Hatua za Makuzi ya Mtoto.

**Muda: Saa 5**

**Malengo Mahsusi**

Baada ya kukamilisha mada ndogo hii, mwanachuo aweze:-

a) Kueleza hatua za ukuaji wa mtoto;
b) Kuainisha makuzi ya mtoto na mabadiliko yanayoambatana na makuzi hayo
c) Kufafanua nafasi ya mwalimu katika malezi ya mtoto kitabia;
d) Kuorodhesha mambo ya kuzingatia katika kila hatua ya ukuaji wa mtoto;
e) Kueleza athari za mazingira na urithi katika ukuaji wa mtoto.

**Mbinu za Kufundishia na Kujifunzia**

a) Majadiliano katika vikundi.
b) Mdahalo.
c) Kazi mradi.

**Vifaa vya Kufundishia na Kujifunzia**

a) Mabango yahusuyo ukuaji wa mtoto.
b) Chati za hatua za ukuaji wa mtoto.
c) Picha zinazoonesha ukuaji wa mtoto.
d) Kadi za kliniki (kadi ya mtoto, kadi ya mama mjamzito).

**Upimaji**

a) Zoezi.
b) Kazi mradi kueleza athari za mazingira na urithi katika ukuaji wa mtoto.
c) Mkoba wa kazi.

## 2.3 Ujana.

**Muda: Saa 4**

**Malengo Mahsusi**

Baada ya kukamilisha mada ndogo hii, mwanachuo aweze:-

a) Kueleza maana ya ujana na mambo muhimu yanayotokea katika kipindi hicho;
b) Kupendekeza njia mbalimbali za kukabiliana na matatizo ya ujana;
c) Kutathmini uhusiano uliopo kati ya makuzi bora ya awali na ukuaji wa mtoto kimwili na kiakili;
d) Kuorodhesha mawakala wa malezi ya vijana na kazi zao.

**Mbinu za Ufundishaji na Ujifunzaji**

a) Bungua bongo.
b) Ziara halisi kutembelea mawakala wa malezi ya vijana ili kupata njia mbalimbali za kukabiliana na changamoto walizonazo vijana.
c) Majadiliano.

**Vifaa vya Kufundishia na Kujifunzia**

a) Kanda za video zihusuzo madawa ya kulevya.
b) Vipeperushi mbalimbali vya mawakala wa malezi ya vijana.
c) Vipeperushi vya kupambana na VVU/UKIMWI.
d) Picha zinazoonesha madhara ya madawa ya kulevya na VVU/UKIMWI.

**Upimaji**

a) Jaribio.
b) Taarifa ya ziara halisi kubaini njia za kukabiliana na changamoto za ujana.
c) Insha ya kielimu kutathmini uhusiano uliopo kati ya makuzi ya awali na ukuaji wa mtoto kimwili na kiakili.

## 3.0 NADHARIA ZA KUJIFUNZA

### 3.1 Dhana ya Kujifunza.

**Muda: Saa 2**

**Malengo Mahsusi**

Baada ya kukamilisha mada ndogo hii, mwanachuo aweze:-

a) Kufafanua maana ya kujifunza;
b) Kueleza umuhimu wa kujifunza;
c) Kuelezea aina za kujifunza
d) Kufafanua nyanja za kujifunza;

**Mbinu za Kufundishia na Kujifunzia**

a) Bungua bongo.
b) Utafiti wa maktaba kuhusu Nyanja, aina za kujifunza na umuhimu wake.
c) Fikiri jozisha shirikisha

**Vifaa vya Kufundishia na Kujifunzia**

a) Vitabu vya Saikolojia ya Elimu
b) Chati/michoro zinazoonesha aina za kujifunza.

**Upimaji**

a) Chemsha bongo.
b) Taarifa ya utafiti wa maktaba.
c) Mkoba wa kazi

## 3.2 Kanuni za Kujifunza

**Muda: Saa 2**

**Malengo Mahsusi**

Baada ya kukamilisha mada ndogo hii, mwanachuo aweze:-

a) Kufafanua kanuni za kujifunza;
b) Kueleza matumizi ya kanuni za kujifunza darasani.

**Mbinu za Kufundishia na Kujifunzia**

a) Majadiliano katika vikundi na mawasilisho kuhusu kanuni za kujifunza (Kanuni ya matokeo, kanuni ya mazoezi na kanuni ya utayari)
b) Igizo dhima kuhusu matumizi ya kanuni za kujifunza.

**Vifaa vya Kufundishia na Kujifunzia**

a) Makala mbalimbali zihusuzo kanuni za kujifunza.
b) Vitabu vya Saikolojia ya Elimu
c) Utafiti wa maktaba/mtandao

**Upimaji**

a) Insha ya kielimu kufafanua kanuni za kujifunza na matumizi yake darasani.
b) Kazi mradi
c) Majaribio, Mazoezi, Kazi za vikundi

## 3.3 Kukumbuka na Kusahau.

**Muda: Saa 3**

**Malengo Mahsusi**

Baada ya kukamilisha mada ndogo hii, mwanachuo aweze:-

a) Kufafanua dhana ya kukumbuka na kusahau;
b) Kueleza misingi ya kukumbuka na kusahau;
c) Kuchambua mambo yanayoathiri kukumbuka;
d) Kueleza mbinu za kujenga kumbukumbu.

**Mbinu za Kufundishia na Kujifunzia**

a) Majadiliano katika vikundi.

b) Ramani ya dhana.

**Vifaa vya Kufundishia na Kujifunzia**

a) Michoro (ramani ya dhana) yenye kuonesha mchakato wa kukumbuka na kusahau.

b) Vitabu vya Saikolojia ya Elimu vyenye mada yakukumbuka na kusahau.

**Upimaji**

a) Jaribio.

b) Kazi binafsi.

### 3.4 Motisho na Vichocheo

**Muda: Saa 3**

**Malengo Mahsusi**

Baada ya kukamilisha mada ndogo hii, mwanachuo aweze:-

a) Kutofautisha motisho na vichocheo katika kujifunza;

b) Kueleza aina za motisho,

c) Kuainisha vichocheo katika kujifunza;

d) Kueleza athari za adhabu katika kujifunza.

**Mbinu za Kufundishia na Kujifunzia**

a) Utafiti wa maktaba na mtandao

b) Majadiliano.

c) Igizo dhima.

d) Mdahalo.

**Vifaa vya Ufundishaji na Ujifunzaji**

a) Makala za Saikolojia (Motisho na Vichocheo)

b) Magazeti na majarida mbalimbali.

c) Kanda za video zenye kuonesha jinsi ya kumotisha.

**Upimaji**

a) Kazi binafsi.

b) Mazoezi, Kazi za vikundi.

c) Jaribio.

## 3.5 Uhawilisho wa Mafunzo

**Muda: Saa 2**

**Malengo Mahsusi**

Baada ya kukamilisha mada ndogo hii, mwanachuo aweze:-

a) Kueleza maana ya kuhawilisha mafunzo

b) Kufafanua aina za kuhawilisha mafunzo.

c) Kueleza kanuni za kuhawilisha mafunzo.

d) Kuchambua umuhimu wa uhawilisho wa mafunzo.

**Mbinu za Kufundishia na Kujifunzia**

a) Bungua bongo.

b) Utafiti wa maktaba kuhusu uhawilisho wa mafunzo, aina na kanuni zake (uhawisho chanya, uhawilisho hasi na uhawilisho butu).

c) Onesho mbinu.

**Vifaa vya Kufundishia na Kujifunzia**

a) Vitabu vya Saikolojia ya Elimu

b) Machapisho mbali mbali ya uhawilisho wa mafunzo

**Upimaji**

a) Maswali ya ana kwa ana.

b) Kazi binafsi.

c) Mkoba wa kazi.

## 4.0. USHAURI NA UNASIHI

### 4.1 Dhana ya Ushauri na Unasihi.

**Muda: Saa 2**

**Malengo Mahsusi**

Baada ya kukamilisha mada ndogo hii, mwanachuo aweze:-

a) Kueleza dhana ya ushauri na unasihi.

b) Kutofautisha ushauri na unasihi.

**Mbinu za Kufundishia na Kujifunzia**

a) Kuorodhesha wanachojua, wanachotaka kujua na watakachojifunza (KWL) juu ya dhana ya ushauri na unasihi.

b) Majadiliano katika vikundi na uwasilishaji.

c) Kualika mgeni kutoa mhadhara kuhusu ushauri na unasihi.

**Vifaa vya Kufundishia na Kujifunzia**

a) Kanda za video zinazoonesha jinsi ya kunasihi,

b) Vitabu vya ushauri na unasihi,

c) Machapisho toka katika magazeti kuhusu unasihi.

**Upimaji**

Kazi binafsi kueleza.

### 4.2 Aina za Kunasihi.

**Muda: Saa 2**

**Malengo Mahsusi**

Baada ya kukamilisha mada ndogo hii, mwanachuo aweze:-

(a) Kueleza aina za unasihi;

(b) Kufafanua umuhimu wa unasihi;
(c) Kuelezea mbinu mbalimbali za unasihi;
(d) Kutofautisha unasihi wa jadi na unasihi wa kisasa.

**Mbinu za Kufundishia na Kujifunzia**

a) Majadiliano.
b) Mhadhara shirikishi.

**Vifaa vya kufundishia na kujifunzia**

a) Vitabu vya ushauri na unasihi
b) Makala mbalimbali za ushauri na unasihi

**Upimaji**

Kazi za vikundi kufafanua aina za unasihi, umuhimu wake na mbinu za kunasihi.

### 4.3 Sifa za Mnasihi.

**Muda: Saa 2**

**Malengo Mahsusi**

Baada ya kukamilisha mada ndogo hii, mwanachuo aweze:-

(a) Kueleza sifa za mnasihi;
(b) Kueleza mambo ya kuzingatia katika kikao cha unasihi;
(c) Kubainisha tofauti zilizopo kati ya mnasihi na mshauri.

**Mbinu za Kufundishia na Kujifunzia**

a) Utafiti wa maktaba/mtandao
b) Mgeni/mtaalamu wa unasihi kueleza mambo ya kuzingatia katika kikao cha kunasihi.

**Vifaa vya Kufundishia na Kujifunzia**

a) Picha za sinema au video zenye maudhui ya mbinu za kunasihi.
b) Vitabu vya ushauri na unasihi.
c) Makala mbalimbali yenye mbinu za unasihi

**Upimaji**

a) Mazoezi.
b) Kazi za vikundi.
c) Kazi binafsi.

## 4.4 Matatizo yanayohitaji Unasihi Shuleni.

**Muda: Saa 4**

**Malengo Mahsusi**

Baada ya kukamilisha mada ndogo hii, mwanachuo aweze:-

(a) Kubainisha matatizo yanayohitaji ushauri nasaha nyumbani na shuleni;
(b) Kueleza wajibu wa wahusika mbalimbali katika kunasihi vijana;
(c) Kufanya zoezi la kunasihi.

**Mbinu za Kufundishia na Kujifunzia**

a) Ziara ya kielimu katika vituo vya watoto yatima, watoto wa mitaani, na shuleni kubaini matatizo yanayohitaji unasihi.
b) Igizo dhima.
c) Maswali na majibu.

**Vifaa vya Kufundishia na Kujifunzia**

a) Vitabu vya ushauri na unasihi.
b) Kanda za video zenye kuonesha vikao vya unasihi.

**Upimaji**

a) Ripoti ya ziara ya kielimu kubaini matatizo yanayohitaji unasihi.
b) Orodha hakiki ya vigezo vya kufanya zoezi la unasihi.

## 5.0 MTAALA

### 5.1 Dhana ya Mtaala

**Muda: Saa 2**

**Malengo Mahsusi**

Baada ya kukamilisha mada ndogo hii, mwanachuo aweze:-

a) Kueleza dhana ya mtaala katika elimu;

b) Kueleza umuhimu wa kuwa na mtaala

c) Kueleza sifa za mtaala;

d) Kubainisha aina za mitaala.

**Mbinu za Kufundishia na Kujifunzia**

a) Maswali na majibu.

b) Majadiliano.

**Vifaa vya Kufundishia na Kujifunzia**

a) Mihtasari ya Elimu ya Msingi

b) Vitabu vya Kiada.

c) Mtaala wa Elimu ya Msingi

**Upimaji**

a) Maswali ya ana kwa ana.

b) Zoezi.

c) Kazi za vikundi.

### 5.2 Vifaa vya Mtaala

**Muda: Saa 4**

**Malengo Mahsusi**

Baada ya kukamilisha mada ndogo hii, mwanachuo aweze:-

a) Kubainisha vifaa vya mtaala;

b) Kuchambua sifa za kila kifaa cha mtaala.

**Mbinu za Kufundishia na Kujifunzia**

a) Fikiri, jozisha na shirikisha.
b) Changanya kete kuchambua sifa za kila kifaa cha mtaala.
c) Bungua bongo.

**Vifaa vya Kufundishia na Kujifunzia**

a) Mihtasari ya Elimu ya Msingi.
b) Vitabu vya Kiada.
c) Kiongozi cha Mwalimu.
d) Vitabu vya rejea.

**Upimaji**

a) Chemsha bongo.
b) Kazi za vikundi.

## 6.0 MATAYARISHO YA UFUNDISHAJI

### 6.1 Dhana ya Matayarisho ya Ufundishaji

**Muda: Saa 2**

**Malengo Mahsusi**

Baada ya kukamilisha mada ndogo hii, mwanachuo aweze:-

a) Kufafanua dhana ya matayarisho ya ufundishaji;
b) Kueleza umuhimu wa matayarisho ya ufundishaji.
c) Kuorodhesha vifaa vinavyohitajika katika matayarisho ya ufundishaji

**Mbinu za Kufundishia na Kujifunzia**

a) Kuorodhesha wanachojua, wanachotaka kujua na watakachojifunza (KWL) kuhusu dhana ya matayarisho ya ufundishaji na umuhimu wake.
b) Bungua bongo juu ya hasara ya mwalimu kufundisha bila matayarisho ya kutosha.
c) Igizo dhima juu ya ufundishaji wenye matayarisho na usio na matayarisho.

**Vifaa vya Kufundishia na Kujifunzia**

a) Mihtasari,

b) Vitabu vya kiada.

c) Machapisho mbalimbali yanayohusu matayarisho ya ufundishaji

**Upimaji**

a) Maswali ya ana kwa ana.

b) Kazi binafsi.

c) Kazi za vikundi.

## 6.2 Azimio la Kazi

**Muda: Saa 4**

**Malengo Mahsusi**

Baada ya kukamilisha mada ndogo hii, mwanachuo aweze:-

a) Kufafanua dhana ya azimio la kazi;

b) Kueleza vipengele vya azimio la kazi;

c) Kutayarisha azimio la kazi.

**Mbinu za Kufundishia na Kujifunzia**

a) Maswali na majibu.

b) Utafiti wa maktaba na mtandao.

d) Majadiliano katika vikundi.

e) Onesho mbinu.

**Vifaa vya Kufundishia na Kujifunzia**

a) Nakala za Maazimio ya Kazi zilizoandaliwa.

b) Kalenda ya mwaka

c) Mihtasari

**Upimaji**

a) Maswali ya ana kwa ana.

b) Mkoba wa kazi.

## 6.3 Andalio la Somo

**Muda: Saa 2**

**Malengo Mahsusi**

Baada ya kukamilisha mada ndogo hii, mwanachuo aweze:-

a) Kueleza dhana ya andalio la somo.
b) Kufafanua vipengele muhimu vya andalio la somo.
c) Kutayarisha andalio la somo kwa kutumia azimio la kazi aliloandaa.

**Mbinu za Kufundishia na Kujifunzia**

a) Majadiliano katika vikundi.
b) Majadiliano katika jozi.
c) Onesho mbinu.

**Vifaa vya Kufundishia na Kujifunzia**

a) Mihtasari.
b) Azimio la kazi,
c) Vitabu vya kiada,
d) Kiongozi cha mwalimu.

**Upimaji**

a) Zoezi.
b) Insha.
c) Mkoba wa kazi.

## 6.4 Nukuu za Somo

**Muda: Saa 3**

**Malengo Mahsusi**

Baada ya kukamilisha mada ndogo hii, mwanachuo aweze:-

a) Kueleza dhana ya nukuu za somo za mwalimu na za mwanafunzi;

b) Kueleza mambo ya kuzingatia katika kutayarisha nukuu za somo za mwalimu na za mwanafunzi;
c) Kutayarisha nukuu za somo aliloandaa;

**Mbinu za Kufundishia na Kujifunzia**

a) Bungua bongo.
b) Mhadhara shirikishi.
c) Onesho mbinu.

**Vifaa vya Kufundishia na Kujifunzia**

a) Mihtasari,
b) Azimio la kazi,
c) Andalio la somo,
d) Vitabu vya kiada,
e) Kiongozi cha mwalimu,
f) Daftari la kutunza nukuu za somo.

**Upimaji**

a) Jaribio.
b) Kazi binafsi.

### 6.5 Shajara la Somo

**Muda: Saa 2**

**Malengo Mahsusi**

Baada ya kukamilisha mada ndogo hii, mwanachuo aweze:-

a) Kufafanua dhana ya Shajara la somo;
b) Kubainisha mambo ya kuzingatia katika kutayarisha shajara la somo;
c) Kuandaa na kujaza shajara la somo la mfano.

**Mbinu za Kufundishia na Kujifunzia**

a) Fikirisha, jozisha na shirikisha.
b) Mhadhara shirikishi.

**Vifaa vya Kufundishia na Kujifunzia**

a) Shajara jipya la somo na lililokwishatumika
b) Mihtasari
c) Vitabu vya kiada
d) Maandalio ya somo

**Upimaji**

(i) Kazi binafsi.
(ii) Mkoba wa kazi.

## 7.0 UFUNDISHAJI

### 7.1 Dhana ya Ufundishaji

**Muda: Saa 2**

**Malengo Mahsusi**

Baada ya kukamilisha mada ndogo hii, mwanachuo aweze:-

a) Kueleza dhana ya ufundishaji;
b) Kufafanua umuhimu wa ufundishaji shirikishi;
c) Kueleza hatua za kufuata katika ufundishaji.

**Mbinu za Kufundishia na Kujifunzia**

a) Bungua bongo.
b) Igizo dhima la ufundishaji shirikishi.
c) Majadiliano.
d) Mdahalo.

**Vifaa vya Kufundishia na Kujifunzia**

a) Chati yenye kuonesha darasa mseto.
b) Vitabu vya rejea na vya kiada.
c) Moduli ya kusimamia darasa mseto.
d) Picha zinazoonesha darasa la watu wazima.

**Upimaji**

a) Zoezi.

b) Kazi mradi.

## 7.2 Misingi ya Ufundishaji

**Muda: Saa 2**

**Malengo Mahsusi**

Baada ya kukamilisha mada ndogo hii, mwanachuo aweze:-

a) Kubainisha misingi ya ufundishaji.

b) Kueleza jinsi misingi ya ufundishaji inavyotumika katika kufundisha na kujifunza.

**Mbinu za Kufundishia na Kujifunzia**

a) Matembezi ya galari kueleza maana, umuhimu na jinsi ya kutumia misingi ya ufundishaji ifuatayo:-
   (i) Kuanza na mada rahisi kwenda ngumu;
   (ii) Kuanza na mada halisi kwenda isiyo halisi.
   (iii) Kuanza na vitendo kwenda nadharia.
   (iv) Kuanza na mada ya kushikika kwenda ya kufikirika.
   (v) Utayari katika kujifunza.

b) Igizo dhima.

**Vifaa vya Kufundishia na Kujifunzia**

a) Vitabu vya Misingi ya Ufundishaji.

b) Chati ya kuonesha misingi ya ufundishaji.

c) Machapisho mbalimbali ya kielimu

**Upimaji**

a) Insha.
b) Mkoba wa kazi
c) Mazoezi

### 7.3 Usimamizi wa Darasa

**Muda: Saa 2**

**Malengo Mahsusi**

Baada ya kukamilisha mada ndogo hii, mwanachuo aweze:-

a) Kueleza maana na umuhimu wa usimamizi wa darasa;
b) Kubainisha mambo ya kuzingatia katika usimamizi wa darasa.

**Mbinu za Kufundishia na Kujifunzia**

a) Bungua bongo.
b) Maswali na majibu.
c) Majadiliano katika vikundi.
d) Igizo dhima.

**Vifaa vya Kufundishia na Kujifunzia**

b) Vitabu vya kanuni za ufundishaji na usimamizi wa darasa.
b) Majarida mbalimbali ya kielimu

**Upimaji**

a) Jaribio.
b) Orodha hakiki.

### 7.4 Njia/Mbinu za Ufundishaji

**Muda: Saa 5**

**Malengo Mahsusi**

Baada ya kukamilisha mada ndogo hii, mwanachuo aweze:-

a) Kufafanua dhana za njia, mbinu na mikakati ya kufundishia na kujifunzia;
b) Kubainisha mbinu mbalimbali za kufundishia na kujifunzia;
c) Kueleza sifa za mbinu za kufundishia na kujifunzia;
d) Kuainisha manufaa na mapungufu ya kila mbinu ya kufundishia na kujifunzia.

**Mbinu za Kufundishia na Kujifunzia**

a) Bungua bongo.
b) Majadiliano.
c) Mdahalo.
d) Changanya kete.

**Vifaa vya Kufundishia na Kujifunzia**

d) Vitini vya maelezo ya mbinu za kufundishia
e) Kiongozi cha mwalimu na vitabu vya kiada.

**Upimaji**

a) Insha
b) Kazi za vikundi

## 7.5 Mazoezi ya Ufundishaji kwa Vitendo

**Muda: Saa 4**

**Malengo Mahsusi**

Baada ya kukamilisha mada ndogo hii, mwanachuo aweze:-

a) Kueleza dhana ya mazoezi ya ufundishaji kwa vitendo;
b) Kufafanua aina ya mazoezi ya ufundishaji;
c) Kubainisha mambo ya kuzingatia katika aina mbalimbali za mazoezi ya kufundisha.

**Mbinu za Kufundishia na Kujifunzia**

a) Bungua bongo.
b) Majadiliano.
c) Changanya kete kiduchu, ufundishaji wa kipindi kimoja.

**Vifaa vya Kufundishia na Kujifunzia**

a) Chati yenye mambo ya kuzingatia katika kufanya maandalizi ya aina zote za mazoezi ya kufundisha.
b) Vitabu vya kiada, nukuu za somo na shajara la somo.
c) Makala mbalimbali ya kielimu

**Upimaji**

a) Maswali ya ana kwa ana.

b) Mkoba wa kazi.

## 8.0 UPIMAJI KATIKA ELIMU

### 8.1 Dhana ya Upimaji wa Kielimu.

**Muda: Saa 2**

**Malengo Mahsusi**

Baada ya kukamilisha mada ndogo hii, mwanachuo aweze:-

a) Kueleza dhana ya Upimaji wa Kielimu;

b) Kubainisha nyanja tatu za Upimaji wa Kielimu.

**Mbinu za Kufundishia na Kujifunzia**

a) Fikirisha, jozisha, shirikisha.

b) Majadiliano katika vikundi.

**Vifaa vya Kufundishia na Kujifunzia**

a) Ripoti za mitihani,

b) Ripoti za wakaguzi wa shule,

c) Fomu ya taarifa ya maendeleo ya mwanafunzi,

d) Machapisho ya maktaba yanayohusu nyanja za kupima katika elimu.

**Upimaji**

a) Chemsha bongo.

b) Insha ya kielimu.

### 8.2 Upimaji na Uwekaji wa Kumbukumbu za Maendeleo ya Mwanafunzi

**Muda: Saa 4**

**Malengo Mahsusi**

Baada ya kukamilisha mada ndogo hii, mwanachuo aweze:-

c) Kueleza njia zinazotumika kupima maendeleo ya mwanafunzi;
b) Kueleza umuhimu wa kuweka kumbukumbu za maendeleo ya mwanafunzi;
d) Kubainisha vipengele muhimu vya kuzingatia katika uwekaji wa kumbukumbu za maendeleo ya mwanafunzi.

**Mbinu za Kufundishia na Kujifunzia**

a) Utafiti wa maktaba na mtandao.
b) Matembezi ya galari .

**Vifaa vya Kufundishia na Kujifunzia**

a) Sampuli ya mazoezi, majaribio na mitihani ya wanafunzi.
b) Sampuli ya fomu za kujaza maendeleo ya mwanafunzi.

**Upimaji**

a) Maswali ya ana kwa ana.
b) Insha.

### 8.3 Utungaji wa Majaribio na Mitihani.

**Muda: Saa 4**

**Malengo Mahsusi**

Baada ya kukamilisha mada ndogo hii, mwanachuo aweze:-

a) Kueleza aina za maswali yanayotumika katika majaribio na mitihani;
b) Kutayarisha jedwali la kutahini;
c) Kutunga maswali ya majaribio na mitihani kwa kutumia jedwali la kutahini;
d) Kutayarisha mwongozo wa usahihishaji wa majaribio na mitihani;
e) Kutumia mwongozo wa kusahihisha majaribio na mitihani.

**Mbinu za Kufundishia na Kujifunzia**

a) Maswali na majibu.
b) Onesho mbinu.
c) Kisa mafunzo.

**Zana /Vifaa vya Kufundishia na Kujifunzia**

a) Sampuli ya majaribio yaliyojibiwa.
b) Mfano wa Jedwali la kutahini lililoandaliwa kwenye kadi ya manila.

**Upimaji**

a) Chemsha bongo.
b) Mkoba wa kazi.

## 8.4 Uchambuzi na Tafsiri ya Matokeo ya Majaribio na Mitihani

**Muda: Saa 5**

**Malengo Mahsusi:**

Baada ya kukamilisha mada ndogo hii, mwanachuo aweze:-

a) Kukokotoa wastani, modi, mfiko na achano sanifu kutokana na alama ghafi za mtihani/jaribio na kufafanua umuhimu wa kila kimoja;
b) Kukokotoa maksi za majaribio na mitihani kwa kutumia kigezo ‘z’;
c) Kurekebisha maksi za majaribio na mitihani kwa kutumia kigezo ‘t’ na kufafanua umuhimu wake;
d) Kutafsiri matokeo ya majaribio na mitihani yaliyorekebishwa.

**Mbinu za Kufundishia na Kujifunzia**

a) Kisa mafunzo.
b) Maswali na majibu.
c) Mdahalo.

**Zana/Vifaa vya Kufundishia na Kujifunzia**

a) Maksi za matokeo ya majaribio na mitihani
b) Kikokotoo.

**Upimaji**

a) Jaribio.
b) Kazi binafsi.
c) Mkoba wa kazi.

## 8.5 Uchanganuzi wa Swali

**Muda: Saa 3**

**Malengo Mahsusi**

Baada ya kukamilisha mada ndogo hii, mwanachuo aweze:-

a) Kueleza dhana ya uchanganuzi wa swali;
b) Kukokotoa uwezo wa upambanuzi wa swali;
c) Kukokotoa kiwango cha ugumu wa swali.

**Mbinu za Kufundishia na Kujifunzia**

a) Bungua bongo.
b) Onesho mbinu.
c) Kisa mafunzo.

**Zana/Vifaa vya Kufundishia na Kujifunzia**

a) Kikokotoo,
b) Sampuli ya Maswali ya majaribio na mitihani.
c) Machapisho mbalimbali kuhusu upimaji wa kielimu

**Upimaji**

a) Zoezi.
b) Kazi za vikundi.

## 9.0 TATHMINI KATIKA ELIMU

### 9.1 Dhana ya Tathmini katika Elimu.

**Muda: Saa 2**

**Malengo Mahsusi**

Baada ya kukamilisha mada ndogo hii, mwanachuo aweze:-

a) Kutofautisha tathmini na upimaji katika elimu.
b) Kueleza umuhimu wa tathmini katika elimu.
c) Kueleza aina za tathmini.

**Mbinu za Kufundishia na Kujifunzia**

a) Mdahalo.
b) Utafiti wa maktaba.

**Vifaa vya Kufundishia na Kujifunzia**

Rejea mbalimbali zinazohusu tathmini katika elimu.

**Upimaji**

a) Kazi binafsi.
b) Zoezi.

### 9.2 Utaratibu wa kufanya Tathmini katika Somo.

**Muda: Saa 3**

**Malengo Mahsusi**

Baada ya kukamilisha mada ndogo hii, mwanachuo aweze:-

a) Kueleza hatua za kufanya tathmini ya somo.
b) Kufanya tathmini ya ufundishaji wa somo.
c) Kuandika ripoti ya tathmini ya somo.
d) Kutumia matokeo ya tathmini katika kuboresha ufundishaji.

**Mbinu za Kufundishia na Kujifunzia**

a) Fikirisha, jozisha na shirikisha.
b) Kisa mafunzo.

**Vifaa vya Kufundishia na Kujifunzia**

a) Fomu za kufanya tathmini ya mazoezi ya kufundisha.
b) Muhtasari wa somo.

**Upimaji**

a) Kazi binafsi.
b) Mazoezi
c) Majaribio.

## 10.0 UTAFITI WA KIELIMU

### 10.1 Dhana ya Utafiti wa Kielimu.

**Muda: Saa 2**

**Malengo Mahsusi**

Baada ya kukamilisha mada ndogo hii, mwanachuo aweze:-

a) Kueleza maana ya utafiti wa kielimu;
b) Kueleza umuhimu wa kufanya utafiti wa kielimu.

**Mbinu za Kufundishia na Kujifunzia**

a) Bungua bongo.
b) Majadiliano vikundi.

**Zana/Vifaa vya Kufundishia na Kujifunzia:**

a) Vitabu mbalimbali vya rejea.
b) Muhtasari wa somo
c) majarida mbalimbali ya kielimu

**Upimaji**

a) Kazi za vikundi.
b) Kazi binafsi.

## 10.2 Hatua za Kufanya Utafiti wa Kielimu.

**Muda: Saa 5**

**Malengo Mahsusi**

Baada ya kukamilisha mada ndogo hii, mwanachuo aweze:-

a) Kufafanua hatua za kufanya utafiti wa kielimu.
b) Kufanya utafiti mdogo wa kielimu kwa kuzingatia hatua zote.

**Mbinu za Kufundishia na Kujifunzia**

a) Majadiliano.
b) Kazi mradi kufanya utafiti mdogo wa kielimu, kuhusu mada mojawapo ya masuala mtambuko katika elimu.

**Zana/Vifaa vya Kufundishia na Kujifunzia**

Sampuli mbalimbali za tafiti za kielimu kutoka maktaba au sehemu nyingine.

**Upimaji**

a) Jaribio.
b) Ripoti ya utafiti mdogo wa kielimu.

## 10.3 Uandishi wa Ripoti ya Utafiti.

**Muda: Saa 5**

**Malengo Mahsusi**

Baada ya kukamilisha mada ndogo hii, mwanachuo aweze:-

a) Kuelezea mpangilio uandishi wa ripoti ya utafiti mdogo wa kielimu;
b) Kuandika ripoti ya utafiti mdogo wa kielimu;
c) Kutumia matokeo ya utafiti katika kuboresha ufundishaji na ujifunzaji.

**Mbinu za Kujifunzia na Kufundishia:**

a) Majadiliano.

b) Matembezi ya ghalari.

c) Kisa mafunzo.

**Vifaa /Zana za Kufundishia na Kujifunzia**

Sampuli mbalimbali za ripoti kutoka maktaba na mtandao

**Upimaji**

a) Chemsha bongo.

b) Kazi mradi.

## 11.0 TAALUMA YA UALIMU

### 11.1 Dhana ya Ualimu.

**Muda: Saa 2**

**Malengo Mahsusi**

Baada ya kukamilisha mada ndogo hii, mwanachuo aweze:-

a) Kueleza dhana ya ualimu;

b) Kueleza sifa za taaluma ya ualimu.

**Mbinu za Kufundishia na Kujifunzia**

a) Maswali na majibu.

b) Mdahalo.

**Zana/Vifaa vya Kufundishia na Kujifunzia**

Rejea mbalimbali, kamusi, “Encyclopedia”.

**Upimaji**

a) Kazi binafsi.

b) Kazi kwa vikundi.

c) Mazoezi

### 11.2 Mafunzo ya Ualimu.

**Muda: Saa 2**

**Malengo Mahsusi**

Baada ya kukamilisha mada ndogo hii, mwanachuo aweze:-

a) Kueleza malengo ya mafunzo ya ualimu Tanzania;
b) Kutathmini mfumo wa mafunzo ya ualimu Tanzania;
c) Kubaini njia mbalimbali za kujiendeleza baada ya kupata mafunzo ya ualimu chuoni.

**Mbinu za Kufundishia na Kujifunzia**

a) Maswali na majibu.
b) Mdahalo.
c) Majadiliano.

**Zana/Vifaa vya Kufundishia na Kujifunzia**

a) Maswali ya mwongozo,
b) Sera ya Elimu na Mafunzo (ETP 1995),
c) Rejea mbalimbali kuhusu mafunzo ya Ualimu

**Upimaji**

a) Jaribio.
b) Zoezi.

### 11.3 Haki na Wajibu wa Mwalimu.

**Muda: Saa 3**

**Malengo Mahsusi**

Baada ya kukamilisha mada ndogo hii, mwanachuo aweze:-

a) Kutofautisha haki na wajibu wa mwalimu kazini;
b) Kubaini wajibu wa mwajiri kwa mwalimu;
c) Kubaini vyombo vinavyosimamia haki na wajibu wa mwalimu kazini.

**Mbinu za Kufundishia na Kujifunzia**

a) Maswali na majibu .
b) Majadiliano.
c) Kualika wageni kutoka TSD, CWT, Mkaguzi wa Shule.

**Zana/Vifaa vya Kufundishia/Kujifunzia**

a) Kanuni za Maadili ya Utumishi wa Walimu,
b) Kitabu cha kanuni za utumishi
c) Sera na Katiba za Vyombo mbalimbali vinavyosimamia haki na wajibu mbalimbali.

**Upimaji**

a) Insha.
b) Maswali ya ana kwa ana.

### 11.4 Changamoto za Ualimu.

**Muda: Saa 2**

**Malengo Mahsusi**

Baada ya kukamilisha mada ndogo hii, mwanachuo aweze:-

a) Kubainisha matatizo yanayomkabili mwalimu katika mazingira ya kazi;
b) Kueleza mbinu mbalimbali za kukabiliana na matatizo ya mwalimu kazini.

**Mbinu za Kufundishia na Kujifunzia**

a) Kazi mradi.
b) Majadiliano.
c) Mgeni (mwalimu mstaafu) kutoa uzoefu wake kuhusu changamoto mbalimbali za walimu na namna ya kukabiliana nazo.

**Zana/Vifaa vya Kufundishia na Kujifunzia**

a) Maswali hojaji,
b) Majarida mbalimbali yanayoonesha changamoto za walimu k.m. majarida ya CWT na Hakielimu.

**Upimaji**

Ripoti ya kazi mradi kuhusu matatizo ya walimu kazini na namna ya kukabiliana nayo.

## 12.0 MAENDELEO YA ELIMU TANZANIA

### 12.1 Dhana ya Elimu.

**Muda: Saa 2**

**Malengo Mahsusi**

Baada ya kukamilisha mada ndogo hii, mwanachuo aweze:-

a) Kufafanua dhana ya elimu;
b) Kutofautisha aina kuu tatu za elimu.
c) Kubainisha mazuri na mapungufu ya aina kuu za elimu

**Mbinu za Kufundishia na Kujifunzia**

a) Kuorodhesha wanachojua, wanachotaka kujua, na watakachojifunza kuhusu dhana ya elimu (KWL).
b) Majadiliano na uwasilishaji kuhusu tofauti za aina kuu tatu za elimu.

**Zana/Vifaa vya Kufundishia na Kujifunzia**

a) Makala mbalimbali ya kielimu,
b) Vitabu vya rejea, kamusi na "Encyclopedia".

**Upimaji**

a) Maswali ya ana kwa ana.
b) Zoezi kutofautisha aina kuu tatu za elimu.

### 12.2 Historia ya Elimu Tanzania.

**Muda: Saa 4**

**Malengo Mahsusi**

Baada ya kukamilisha mada ndogo hii, mwanachuo aweze:-

(a) Kubaini vipindi mbalimbali vya Historia ya Elimu Tanzania;

(b) Kuchambua sera zilizoongoza elimu katika vipindi mbalimbali;

(c) Kuchambua misingi mikuu ya Elimu ya Kujitegemea.

**Mbinu za Kufundishia na Kujifunzia**

a) Majadiliano, uwasilishaji na mhadhra shirikishi kubaini vipindi vikuu katika historia ya elimu ya Tanzania:
- Elimu kabla ya ukoloni.
- Elimu wakati wa ukoloni (Kiarabu, Kijerumani na Kiingereza).
- Elimu baada ya Uhuru.
- Elimu baada ya Azimio la Arusha.

b) Utafiti wa maktaba na mtandao kulinganisha falsafa ya Elimu ya Kujitegemea na falsafa nyingine.

**Zana/Vifaa vya Kufundishia na Kujifunzia**

a) Makala mbalimbali ya kielimu,
b) Chati zinazoonyesha vipindi mbalimbali katika historia ya elimu Tanzania na sera zake.
c) Vitabu vya rejea,

**Upimaji**

a) Jaribio.
b) Taarifa ya utafiti kulinganisha falsafa ya Elimu ya Kujitegemea na falsafa nyingine.

## 13.0 UONGOZI WA ELIMU TANZANIA

### 13.1 Dhana ya Uongozi wa Elimu.

**Muda: Saa 1**

**Malengo Mahsusi**

Baada ya kukamilisha mada ndogo hii, mwanachuo aweze:-

a) Kueleza maana ya Uongozi;

b) Kufafanua aina za Uongozi;

c) Kueleza dhana ya Uongozi wa Elimu.

**Mbinu za Kujifunzia na Kufundishia**

a) Maswali na majibu.

b) Mhadhara shirikishi.

c) Fikirisha, jozisha na shirikisha.

**Zana/Vifaa vya Kufundishia/Kujifunzia**

Rejea mbalimbali.

**Upimaji**

a) Maswali ya ana kwa ana.

b) Zoezi.

c) Majaribio

### 13.2 Ngazi za Uongozi wa Elimu na Mahusiano.

**Muda: Saa 3**

**Malengo Mahsusi**

Baada ya kukamilisha mada ndogo hii, mwanachuo aweze:-

a) Kubainisha ngazi mbalimbali katika muundo wa Uongozi wa Elimu Tanzania.

b) Kuelezea majukumu ya Viongozi katika ngazi mbalimbali za Uongozi wa Elimu.

c) Kubainisha mapungufu ya uongozi wa elimu katika ngazi mbalimbali

**Mbinu za Kufundishia na Kujifunzia**

a) Mdahalo.
b) Mhadhara shirikishi.
c) Majadiliano.

**Zana/Vifaa vya Kufundishia na Kujifunzia**

a) Chati inayoonesha muundo wa uongozi wa elimu,
b) Nyaraka za elimu

**Upimaji**

a) Insha

b) Kazi za vikundi

## 14.0 ELIMU JUMUISHI

### 14.1 Dhana ya Elimu Jumuishi.

**Muda: Saa 1**

**Malengo Mahsusi**

Baada ya kukamilisha mada ndogo hii, mwanachuo aweze:-

a) Kueleza maana ya elimu jumuishi;
b) Kufafanua umuhimu wa elimu jumuishi.

**Mbinu za Kufundishia na Kujifunzia**

a) Bungua bongo.
b) Majadiliano katika vikundi.

**Zana/Vifaa vya Kufundishia na Kujifunzia**

a) Kamusi,
b) Vitabu mbalimbali,
c) Majarida mbalimbali.
d) Makala mbalimbali zilizosambazwa kutoka katika mtandao/tovuti.

**Upimaji**

Kazi za vikundi .

### 14.2 Utekelezaji wa Elimu Jumuishi.

**Muda: Saa 4**

**Malengo Mahsusi:**

Baada ya kukamilisha mada ndogo hii, mwanachuo aweze:-

a) Kubaini wanafunzi wenye mahitaji maalum;
b) Kuelezea namna ya kujumuisha wanafunzi wenye mahitaji mbalimbali yanayoonekana na yasiyoonekana kwa macho.
c) Kuelezea umuhimu wa utekelezaji wa Elimu Jumuishi

**Mbinu za Kufundishia na Kujifunzia**

a) Ziara kubaini wanafunzi wenye mahitaji maalum.
b) Majadiliano kuhusu namna ya kujumuisha wanafunzi wenye mahitaji maalum.

**Zana / vifaa vya Kufundishia na Kujifunzia**

a) Shajara
b) Hojaji
c) Orodha hakiki.

**Upimaji**

a) Taarifa ya ziara kubaini wanafunzi wenye mahitaji maalum.
b) Kazi za vikundi kuhusu namna ya kujumuisha wanafunzi wenye mahitaji maalum.

### 14.3 Changamoto za Elimu Jumuishi.

**Muda: Saa 2**

**Malengo Mahsusi**

Baada ya kukamilisha mada ndogo hii, mwanachuo aweze:-

a) Kubaini changamoto za elimu jumuishi;
b) Kueleza njia za kukabiliana na changamoto za elimu jumuishi.

**Mbinu za Kufundshia na Kujifunzia**

a) Majadiliano katika makundi.
b) Onesho mbinu.
c) Bungua bongo.

**Zana/Vifaa vya Kufundishia na Kujifunzia**

a) Chati inayoonesha muhtasari wa changamoto na utatuzi wake,
b) Majarida mbalimbali.

**Upimaji**

a) Kazi binafsi.
b) Majaribio.

## 15.0 ELIMU YA WATU WAZIMA

### 15.1 Dhana ya Elimu ya Watu Wazima.

**Muda: Saa 2**

**Malengo Mahsusi**

Baada ya kukamilisha mada ndogo hii, mwanachuo aweze:-

a) Kueleza maana ya Elimu ya Watu Wazima.
b) Kufafanua sifa na mahitaji ya Mwanafunzi mtu mzima.
c) Kueleza umuhimu wa Elimu ya Watu Wazima.

**Mbinu za Kufundishia na Kujifunzia**

a) Bungua bongo.
b) Kumwalika Mgeni/mtaalam wa elimu ya watu wazima kufafanua sifa na mahitaji ya mwanafunzi mtu mzima.
c) Majadiliano.

**Zana/Vifaa vya Kufundishia na Kujifunzia**

a) Vipeperushi na machapisho mbalimbali,
b) Mabango yanayoonesha shughuli za elimu ya watu wazima,
c) Moduli za Elimu ya Watu Wazima.

**Upimaji**

a) Maswali ya ana kwa ana.
b) Kazi binafsi
c) Mazoezi, majaribio

**15.2 Uendeshaji wa Elimu ya Watu Wazima.**

**Muda: Saa 3**

**Malengo Mahsusi**

Baada ya kukamilisha mada ndogo hii, mwanachuo aweze:-

a) Kueleza mikakati ya Utekelezaji wa Elimu ya Watu Wazima Tanzania;
b) Kuelezea muundo wa uendeshaji wa Elimu ya Watu Wazima Tanzania;
c) Kutofautisha uendeshaji wa Kisomo Chenye Manufaa (KCM) na Kisomo cha Kujiendeleza (KCK).

**Mbinu za Kufundishia na Kujifunzia**

a) Ziara halisi kubaini mikakati ya utekelezaji wa elimu ya watu wazima na tofauti kati ya Kisomo Chenye Manufaa na Kisomo cha Kujiendeleza.
b) Kumwakilisha Mgeni/mtaalam wa Elimu ya Watu Wazima kutoa mhadhara shirikishi kuhusu muundo na uendeshaji wa Elimu ya Watu Wazima Tanzania.

**Zana/Vifaa vya Kufundishia na Kujifunzia**

a) Vipeperushi na machapisho mbalimbali,
b) Mabango, chati zinazoonesha muundo.

**Upimaji**

a) Taarifa ya ziara kubaini mikakati ya utekelezaji wa elimu ya watu wazima na tofauti kati ya Kisomo Chenye Manufaa na Kisomo cha Kujiendeleza.
b) Jaribio.

## Rejea Zilizotumika


MOEC (1997): **Curriculum and Teaching Syllabus for Diploma in Education,** Dar es Salaam, Tanzania.

MOEC (1997): **Syllabus for Diploma in Education: Foundation of Education, Educational Research, Measurement and Evaluation Educational Psychology, Guidance and Counseling.** Dar es Salaam, Tanzania.

MOEVT (2007) **Foundations of Education Syllabus for Diploma in Secondary Education,** Dar es Salaam, Tanzania

MOEVT (2007): **Educational Psychology, Guidance and Counseling, Syllabus for Diploma in Secondary Education,** Dar es Salaam, Tanzania.

MOVET (2007): **Educational Research, Measurement and Evaluation Syllabus for Diploma in Secondary Education** Dar es Salaam, Tanzania

Neary, M. (2002): **Curriculum Studies in Post-compulsory and Adult Education:** A Teacher's and Student Teacher's Study Guide. Nelson Thornes Ltd, Cheltenham. UK.

Taasisi ya Elimu Tanzania (1994) **Ukuzaji Mitaala na Unasihi**. TIE, Dar es Salaam

Taasisi ya Ukuzaji Mitaala (1992) **Saikolojia ya Elimu.** WEU, DSM

TIE (2003) **Moduli ya Somo la Misingi ya Elimu:** Mafunzo ya Ualimu Ngazi ya Cheti, Dar es Salaam, Tanzania

TIE (2003) **Moduli ya Somo la Saikolojia na Unasihi Mafunzo ya Ualimu ngazi ya Cheti,** Dar es Salaam, Tanzania

TIE (2003) **Moduli ya Somo la Upimaji, Tathmini na Utafiti: Mafunzo ya Ualimu Ngazi ya Cheti**. Dar es Salaam, Tanzania.

Wizara ya Elimu na Utamaduni (1997): **Muhtasari wa Misingi ya Elimu,** Dar es Salaam, Tanzania

Wizara ya Elimu na Utamaduni (2003): **Muhtasari wa Misingi ya Elimu: Mafunzo ya Ualimu ngazi ya Cheti,** Dar es Salaam Tanzania

Wizara ya Elimu na Utamaduni (2003): **Muhtasari wa Mitaala na Ufundishaji: Mafunzo ya Ualimu ngazi ya Cheti,** Dar es Salaam, Tanzania

Wizara ya Elimu na Utamaduni (2003): **Muhtasari wa Saikolojia ya Elimu na Unasihi Mafunzo ya Ualimu ngazi ya Cheti,** Dar es Salaam, Tanzania

Wizara ya Elimu na Utamaduni (2003): **Muhtasari wa Upimaji, Tathmini na Utafiti: Mafunzo ya Ualimu ngazi ya Cheti**. Dar es Salaam, Tanzania